FOUNTAIN OF IDEAS

chemchemi

KIGODA CHA UPROFESA CHA MWALIMU NYERERE

Bodi ya Wahariri na Shukrani

Wasemavyo Wahariri 1

Makala

Haja na Namna ya Kutoa Elimu ya Uraia Tanzania 3
Bashiru Ally

Uliberali-Mamboleo Ndani ya MKUKUTA 8
Opportuna Kweka

Uliberali-Mamboleo ni nini? Uchambuzi Mfupi wa Makala ya Kweka ya Uliberali-Mamboleo Ndani ya MKUKUTA 15
Adolf Mkenda

Juu ya Mahakama ya Kadhi (Tafsiri na Muhtasari wa Kijitabu cha Hamidu Ismail Majamba Kiitwacho Uwezekano na Mantiki ya Kuanzisha Mahakama ya Kadhi Tanzania Bara) 18
Aldin K. Mutembei

Edward Moringe Sokoine na Mapinduzi Vijijini . 23
Issa G. Shivji

Ubidhaishaji wa Elimu ya Awali Chini ya Uliberali-Mamboleo 27
Jacqueline Mgumia

'Sanaa kwa Maendeleo' ya Jamii au Uliberali? . 31
Vicensia Shule

Kumbukizi: Wasifu wa Prof. Haroub Miraji Othman [1942 - 2009] 35
Chris Maina Perter

Kumbukizi: Ndugu Yangu, Rafiki Yangu, (Shairi) Kamaradi Harubu 39
Issa Shivji

Mawazo ya Awali Kuhusu Namna ya Kujenga au Kubomoa Utamaduni wa Usomaji 40
F. E. M. K. Senkoro

Malumbano na Migongano ya 'Wakwasi' na Madhila ya Wanyonge Tanzania 43
Ng'wanza Kamata

Ulimbikizaji wa Mtaji kwa Unyang'anyi Chini ya Ubeberu Nchini Tanzania 48
Abunuwasi L. Mwami

Maongezi

Maongezi Juu ya Muungano: Issa Shivji na Bernadeta Killian, Chris Peter, Ismail Jussa, Mohamed Bakari, Ng'wanza Kamata na Adolf Mkenda 56
Jacqueline Mgumia

Mazungumzo kati ya Kingunge Ngombale-Mwiru na Issa Shivji 64
Jacqueline Mgumia na Washikala Malango

Kutoka Katika Historia

Miongozo Miwili ya Chama na Tabaka Lililopindua Ujamaa 80
Issa Shivji

Sheikh Amri K. Abeid ni Nani? 82
Adolf Mkenda

Mashairi

Tanzania! Tanzania! 78
Mwalimu Julius Nyerere

Mbona Tunazama? 79
Karola Kinasha

Nukuu Kutoka kwa Mwalimu

Kuhusu Kupokezana Uraisi 79

Kuhusu Muungano na Ubaguzi 79

Mapitio ya Kitabu

Maisha na Nyakati za Abdulahid Sykes (1924 - 1968): Historia Iliyofichwa Kuhusu Harakati za Waislam Dhidi ya Ukoloni wa Waingereza Katika Tanganyika 83
Adof A. Mkenda

OKTOBA 2009 | TOLEO NA. 2 | ISSN 1821-7036

BODI YA UHARIRI

BODI YA UHARIRI
Issa Shivji (Mhariri Mkuu)
Adolf Mkenda
Opportuna Kweka

MHARIRI MSAIDIZI
Jacqueline Mgumia

AFISA UTAWALA MSAIDIZI
Walter Rodney Luanda

Vicensia Shule
2009

Vicensia Shule
P. O. Box 35594
Dar es Salaam
Tanzania
www.vicensiashule.com

KIGODA CHA UPROFESA CHA MWALIMU NYERERE
KATIKA PAN-AFRICAN STUDIES
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
S.L.P. 35091
Dar es Salaam

SIMU: 255-(0) 22 – 2410763
PEPE: mwalimunyererechair@udsm.ac.tz
TOVUTI: www.nyererechair.ac.tz

JARIDA HILI LIMECHAPISHWA NA:
Mkuki na Nyota kwa niaba ya Kigoda cha Mwalimu

MHARIRI WA MATINI: F.E.M.K. Senkoro

USANIFU WA JALADA: Spearhead LTD

USANIFU WA MAANDISHI: Fraternus T. Lyimo

Tunawashukuru ...

Hili ni jarida linalotolewa na Kigoda cha Taaluma cha Mwalimu Nyerere cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Jarida hili hutoka mara mbili kwa mwaka. Toleo moja hutoka kwa lugha ya Kiingereza mwezi wa nne wakati wa kumbukumbu ya kuzaliwa kwa Mwalimu. Kumbukumbu hii huadhimishwa kwa Tamasha la Kitaaluma la Kigoda cha Kitaaluma cha Mwalimu Nyerere ambamo toleo la Chemchemi la mwaka huo hutolewa rasmi. Toleo jingine hutolewa kwa Kiswahili mwezi wa kumi wakati wa kumbukumbu ya kifo cha Mwalimu Nyerere. Kigoda cha Kitaaluma cha Mwalimu Nyerere huadhimisha kumbukumbu hii kwa kuendesha Mbongi wa Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kwa kuchapisha toleo la Kiswahili la Chemchemi.

Bodi ya Wahariri inayo furaha kubwa kuwaletea toleo hili la pili la Chemchemi na ambalo ni la kwanza kwa lugha ya Kiswahili. Uchapishaji wa toleo hili umewezeshwa kwa msaada wa fedha kutoka CODESRIA, shirika lenye makao makuu huko Dakar, Senegal, na ambalo limejipatia umaarufu mkubwa kwa kugharamia tafiti na machapisho mbali mbali ya kimaendeleo katika bara la Afrika. Tunaishukuru Kamati ya Utendaji ya CODESRIA kwa kukubali kwa moyo mmoja kukiunga mkono Kigoda cha Mwalimu Nyerere ikiwa ni pamoja na kutoa fedha kugharamia uchapishaji wa toleo hili.

Professor Senkoro wa Taasisi ya Taaluma za Kiswahili ya ChuoKikuu cha Dar es Salaam alifanya uhariri wa lugha kwa baadhi ya makala za toleo hili; tunamshukuru sana. Mkuki na Nyota wamechapisha toleo hili kwa niaba ya Kigoda cha Mwalimu Nyerere kwa kupitiliza hata majukumu ya kawaida ya wachapishaji ili tuu kukidhi mahitaji yetu mengi ikiwa ni pamoja na suala la kufukuzana na muda. Fraternus Lyimo wa Mkuki na Nyota ndiye aliyetengeneza mpangilio wa makala zilizomo humu kwa ajili ya uchapishaji. Kwa hakika imekuwa ni faraja kwetu kufanya kazi na Mkuki na Nyota.

Tunamshukuru sana Karola Kinasha sio tuu kwa kuturuhusu kuchapisha humu kwenye jarida letu beti za nyimbo yake maarufu iitwayo "Mbona Tunazama", bali pia kwa kuturuhusu kunakili kwenye CD wimbo wake huu wa kusisimua na hivyo kutuwezesha kuweka CD hii katika kila nakala ya jarida hili. Wimbo huu ulitungwa mahsusi na Karola kwa ajili ya Wiki ya Tamasha la Kitaaluma la Mwalimu Nyerere lililofanyika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kati ya tarehe 13 na 17 Aprili mwaka huu. Wimbo huu uliimbwa hadharani kwa mara kwanza kabisa kwenye Ukumbi wa Nkrumah wakati wa Tamasha. Ahsante sana Karola. Tunatumaini wasomaji watafurahia wimbo huu wenye maudhui mazito na wa kiwango cha juu cha usanii. Tunawashukuru wote walioandika makala kwenye jarida hili, na hasa Dr. Aldin Mutembei ambaye alikubali ombi letu la kutafsiri na kufupisha kitabu cha Dr Hamidu Majamba juu ya suala la mahakama ya Kadhi, na pia tunamshukuru Dr. Majamba kwa kutoa kibali tafsiri na muhtasari huu alio uhakiki mwenyewe utumike kwenye jarida hili.

Chemchemi ni jarida la kuchokoza mawazo ya kitaaluma na kuamsha mijadala ya kimaendeleo. Kila mtu anakaribishwa kutoa makala yake.

ambapo Serikali imetoa agizo kwa uanzishwaji wa shule za kata. Leo hii shule zimejegwa kwa hamasa lakini kunauhaba wa walimu, vifaa vya kufundishia, na bajeti ya kuhakikisha shule zinajiendesha vizuri. Ni ukweli usiopingika kwamba uanzishwaji wa shule hizi utaongeza gharama kwa Serikali na wazazi, lakini gharama zake zisiifanye Serikali kukimbia jukumu la kusomesha. Kutatua tatizo hili serikali inaweza kutenga asilimia fulani ya kodi kwa lengo la kujenga mfumo wa awali kwa wote. Kwa njia hiyo, wananchi watahamasika na kuanza kuhoji, na huo ndio utakuwa mwanzo wa elimu bora ya awali na kwa wote.

Marejeo

Cummins, J. (2000). Language, power, and pedagogy. Bilingual children in the crossfire. Clevedon, England: Multilingual Matters

Mbugua Tata J. (2004) Early Childhood Care and Education in Kenya, Childhood Education, Vol. 80 –

MOEC, Ministry of Education and Culture(1995): Education and Training Policy, Dar es Salaam

Nyerere, J.K. (1979): President's Speech on the International Year of the Child in UNICEF .

Omari, I.M. (1973): "Child Care and the Child Welfare" in UNICEF/ Tanzania National Scientific Research Council: The Young Child in Tanzania. Dar es Salaam: UNICEF, Dar es Salaam Office.

Seif, B.T (1991): A State of the Art Review on Pre-school Education and Care in Mainland Tanzania, Dar es Salaam: MOEC.

Senkoro, F.E.M.K. (2008) "Mauaji ya Halaiki ya Watoto wa Tanzania Kupitia Lugha ya. Kufundishia Sekondari na Vyuoni"

Wizara ya Elimu, Muhtasari wa Elimu ya Awali (1990) na Mwongozo wa Shule za Awali (1991) Dar es Salaam

Skutnabb-Kangas, T. (2000). Linguistic genocide in education-or worldwide diversity and human rights? Mahwah, NJ: Lawrence Erlbaum Associates

'Sanaa kwa Maendeleo' ya Jamii au Uliberali?

Vicensia Shule
Idara ya Sanaa na Sanaa za Maonyesho
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
vicensiashule@yahoo.com

Sanaa kwa Maendeleo (SKM) ni dhana ya kutumia sanaa hasa za maonyesho ili kumwezesha mwanajamii kujiletea maendeleo yake mwenyewe. Mbinu ya SKM kwa kiasi kikubwa imejikita katika kuamini kuwa ikiwa jamii fulani ina matatizo ya kimaendeleo, ni wanajamii wenyewe ndio wenye uwezo wa kuyajadili na kuyapatia ufumbuzi. Ingawa dhana hii siyo ngeni masikioni mwa wanajamii na wanaharakati wa maendeleo, imekuwa ikitumika kama kielelezo kuonesha mchango wa sanaa katika kuleta maendeleo kwa Mtanzania, Mwafrika na sehemu nyingine duniani ambako imekuwa ikitumika.

Lengo la makala hii ni kuangalia undumilakuwili wa SKM katika miradi ya maendeleo inayofadhiliwa na wafadhili toka nje hasa katika miradi inayojihusisha na maendeleo katika jamii ya Tanzania ya leo. Kimsingi sanaa ni chombo makini cha kuionesha jamii kama ilivyo (simulacrum). Carlson (2001) anasisitiza hilo kwa kuonesha umuhimu wa sanaa za maonyesho katika kuweka sawa utamaduni na historia ya jamii. Hivyo basi ni dhahiri kuwa sanaa za maonyesho ni mhimili muhimu katika mfumo wa maisha ya binadamu. Kutokana na nadharia hiyo hiyo, SKM ilionekana kuwa 'zao' la jamii kulingana na uwezo wake wa kutumia fani mbalimbali za sanaa za maonyesho zilizopo katika jamii husika kama vile ngoma, hadithi, maigizo, nyimbo, mashairi, miviga na nyinginezo. Fani hizi ndio msingi wa kuwepo kwa sanaa za maonyesho katika jamii nyingi za Kiafrika.

Kama ilivyoainishwa katika vitabu, majarida na machapisho mbalimbali, SKM ilianza kutumika Tanzania mwishoni mwa miaka ya 1970 na mwanzoni mwa miaka ya 1980 (Mlama,1991). Ulikuwa ni wakati ambao Tanzania ilikuwa inakabiliwa na kipindi kigumu kiuchumi, ingawaje mikwamo ya kiuchumi inaendelea hadi sasa. Watanzania walikuwa ndio kwanza wametoka kwenye Operesheni Vijiji, ikafuata Vita ya Kagera ya mwaka 1978/79. Vilevile kulikuwa na mfumuko wa bei ya mafuta ulimwenguni, njaa, na, mbaya zaidi, sera gandamizi za Mfuko wa Fedha wa Kimataifa (IMF) na Benki ya Dunia zililazimishwa kutumika kama njia pekee ya kuunusuru uchumi. (Chachage & Chachage, 2003). Wakati huo tulikuwa tunaambiwa "Chama Kimeshika Hatamu". Kutokana na hali halisi ya Watanzania walilazimika kuhoji uhalali wa utendaji usioridhisha wa serikali ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) iliyokuwa madarakani wakati wa harakati za kujenga nchi ya Ujamaa na Kujitegemea. Hivyo basi, fursa za kuhoji uhalali wa sera na viongozi walioshindwa kuleta maendeleo zilikuwa adimu.

Wataalamu wa sanaa kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wakiongozwa na Amandina Lihamba, Penina Mlama na marehemu Eberhardt Chambulikazi, kama waasisi wa SKM nchini Tanzania, walijaribu kutumia sanaa kama njia ya kutafuta suluhisho kwa changamoto zilizokuwa zinaikabili

jamii. Lengo hasa lilikuwa ni kuiwezesha sanaa kutumika katika kusukuma gurudumu la maendeleo (Eyoh, 1984, Kerr, 1995). SKM ililenga kuhakikisha kuwa maendeleo yanatoka kwa watu na kwa manufaa yao. Ndio maana hadi leo SKM inafahamika kama sanaa ya watu, kwa ajili ya watu toka kwa watu, kwenda kwa watu. Hivi sasa SKM imefanikiwa 'kupachikwa' katika mikakati mbalimbali kwa sifa yake ya kuwa mbinu shirikishi. Vilevile kwa kiasi kikubwa SKM imekuwa ikitumika kama njia mojawapo ya kufanyia utafiti ili kupata taarifa zitakazosaidia kuboresha maisha ya wanajamii. Kutoka na na mafanikio ya SKM kwa kipindi cha miaka ya 1980 hadi mwishoni mwa 1990 tunaweza kusema kuwa SKM ni kati ya mbinu zinazoweza kuwapa wanajamii fursa kuntu ya kuyachambua maisha yao kulingana na mazingira wanayoishi, huku wakiburudika. Pia ni mbinu ya kimapinduzi iwezayo kuwanyang'anya 'hatamu' viongozi wazembe pale wanajamii wanapopata fursa ya kuchangia hoja na kufanya maazimio yao. Mlama (1991) amechambua baadhi ya warsha za SKM zilizoleta mafanikio makubwa, mfano ni zile za Malya-Mwanza (1982), Msoga-Pwani (1983) na Mkambalani-Morogoro (1986). Hadi hivi sasa warsha zilizokwishafanyika ni nyingi zisizokuwa na idadi. Chache zimepata nafasi ya kuwekewa kumbukumbu na nyingine nyingi 'zimeishia hewani' baada ya kufanyika. Vilevile wataalamu wengine kwa kuonesha manufaa na mafanikio ya SKM, wemetoa wito wa matumizi ya mbinu hii ili kuharakisha maendeleo (Bakari & Materego, 2008; Etherton, 2004; Eyoh, 1984).

SKM hufanyika kwa kupitia hatua mbalimbali. Kwa mujibu wa Bakari & Materego (2008) zipo hatua tisa. Kwanza ni kuchagua jamii ambayo SKM itafanyika. Pili ni kuyazoea mazingira, tatu ni kufanya utafiti wa matatizo. Nne, ni kuchambua matatizo yaliyojitokeza. Hatua ya tano ni uundaji sanaa na sita ni maonyesho. Baada ya hapo majadiliano hufuata, kisha tathmini hufanyika na mwisho kabisa ni ufuatiliaji. Hatua ya pili hadi ya nane huweza kufanyika katika kipindi cha siku saba au zaidi kulingana na mpangilio mzima wa SKM. Tathmini inayofanyika hapa ni ya awali, mara tu baada majadiliano. Ufuatiliaji hufanyika kulingana na maazimio yaliyopitishwa na mara nyingi hufanyika baada ya miezi sita, mwaka au hata miaka. Wakati mwingine tathmini haifanyiki kabisa na nitafafanua sababu mbalimbali za hali hiyo.

Katika kutumia SKM waraghibishi/ wawezeshaji kutoka nje ya jamii wakishirikiana na wanajamii hupitia hatua zote. Wanajamii wenyewe ndio wanaochukua jukumu la kuendesha mijadala wakati au baada ya maonyesho. Kimsingi SKM imejikita katika kutumia waraghibishi toka nje ya jamii husika kwa lengo la kuwajengea uwezo waraghibishi wa ndani ili waweze kuendeleza mchakato wa SKM pale wawezeshaji toka nje ya jamii watakapoondoka. Ripoti mbalimbali zimeonesha kuwa mara nyingi SKM huishia pale waraghibishi kutoka nje wanapoondoka. Hii inatokana na ukweli kuwa ingawa SKM ni mali ya jamii, inayofanywa na wanajamii, toka katika jamii, kwa ajili ya jamii; umiliki wake uko mikononi mwa wanaotoa wazo na fedha za kuendesha mchakato huo katika jamii fulani. (Materego,2002).

Kwa muda mrefu SKM imekuwa ikipata ufadhili kutoka kwenye mashirika ya kimataifa. Hapa tunazungumzia 'ufadhili mkubwa' wa fedha za kuweza kuleta wazo la kufanya SKM katika jamii fulani. Ukweli unabaki kuwa Nyerere kama alivyonukuliwa na Lihamba (1985) alionya mapema kuwa, mtu huwezi kuwa unategemea ufadhili na bado ukabaki huru. Ufadhili, zawadi na mikopo toka nje inahatarisha uhuru wa Watanzania. Na ikiwa ni kupata maendeleo, wanajamii wenyewe ndio wanaotegemewa kuchukua jukumu la maendeleo na siyo kutegemea wafadhili. Nyerere (1968) pia ameonesha kuwa hakuna tofauti yoyote kati ya uhuru na utumwa pale unapotegemea ufadhili kwa sababu 'anayemlipa mpiga zumari, ndiye anayechagua wimbo'.

Hivi sasa kumeibuka matumizi mapya ya SKM. Miradi mingi inayolenga maendeleo imelazimishwa kutumia sera za utamaduni na mbinu shirikishi (Diagne & Ossebi, 1996). Ndagala (2007) anatuambia kuwa hata Benki ya Dunia sasa nayo imetambua umuhimu wa utamaduni na maendeleo. Kwa kuwa SKM ni moja kati ya mbinu shirikishi, imekuwa ikipachikwa katika miradi inayofadhiliwa na mashirika hayo. Changamoto iliyopo ni kuwa mfumo wa dunia umetawaliwa na ubepari, ubeberu na uliberali mamboleo hivyo siyo rahisi kwa mfadhili kuja kumsaidia Mtanzania kujikwamua bila kuwa na malengo. Amartya Sen amesema wazi kuwa, ulimwengu wa mabenki na ule wa utamaduni hauna mambo mengi yanayolandana. Hivyo si rahisi kuweka dhana hizi mbili (ulimbikizaji wa mtaji na utamaduni) kwenye kapu moja. Tunaambiwa kuwa sasa hivi wafadhili nao wanakuja kwa msukumo wa kibinaadamu kumletea Mwafrika maendeleo, msukumo ambao uliwaleta wamisionari wakati wa ukoloni kuja kukomesha biashara ya utumwa na kumstaarabisha Mwafrika. Maendeleo haya kupitia mipango ya maendeleo ya uchumi ya Mfuko wa Fedha wa Dunia na Benki ya Dunia (kama vile SAPs na mingine) yanalazimisha watu kuamini kuwa kupitia utandawazi 'dunia sasa ni kijiji'. Shivji (2007) anatuonya tusibweteke kwani uliberali mamboleo unawakilisha shari ya kurudi kwa ubeberu katika mfumo wa utandawazi. Ni lazima kutia

shaka maendeleo yanayoshinikizwa kupitia utandawazi.

Tangu kuanza kutumika kwa mbinu ya SKM, kumekuwa na mabadiliko mengi ya kiutendaji na kiitikadi. Dhana ya maendeleo ya watu toka kwa watu kwa manufaa ya watu, imemezwa na sera za wafadhili. Miradi inayoandikwa ni lazima iende sambamba na sera za wafadhili na hata za dola, hata kama hazimsaidii Mtanzania. Jane Plastow (2009) anajaribu kuhoji umuhimu wa SKM katika Afrika ya leo, kama kweli ni mbinu ya kuwawezesha wanajamii au ni zana ya kuwagandamiza. Pia anahoji iwapo waraghibishi wa SKM wako makini katika kutumia mbinu hii wanapoiandika katika miradi yao au suala la msingi ni kuangalia fedha za wafadhili na jinsi ya kuzipata. Kwa ujumla Plastow anaona SKM kama biashara, utaratibu wa kumyang'anya uwezo mwanajamii na zana jadidi ya kumgandamiza. Kimsingi mchakato wa SKM umejikita katika kuiangalia jamii kutoka juu na mara nyingi unashindwa kuiwezesha jamii katika ngazi ya chini kabisa (Materego, 2002). SKM ya sasa hivi haiwajali wanajamii, bali inazingatia kuwa ujumbe uliotolewa na mfadhili umefika. Wakati mwingine hata kama ujumbe huo hauendani na mtazamo au hautatui matatizo ya jamii husika, utapachikwa katika SKM na kuwasilishwa. Wakati wa kuandika ripoti ni wazi kuwa wenye mradi wataonesha kuwa maoni na mawazo yaliyotolewa ni ya wanajamii kwani wametumia mbinu shirikishi kuyapata.

Kwa upande wa sanaa, SKM imegeuka kuwa njia moja wapo ya kuififisha na kuinyang'anya jamii amali yake. Kuendelea kutumia SKM kwa lengo la kufikisha ujumbe tu ni dhahiri mizania ya dhima nyingine za sanaa kama burudani na umbuji zimemezwa. Hali hii haina tofauti na sanaa za kisiasa, sanaa za kipropaganda na zile zinazolenga soko (sanaa za biashara). Kumekuwa na wasiwasi kuwa kuendelea kutumia sanaa zisizosanifishwa katika SKM ni kushusha hadhi ya sanaa za maonyesho. Kiujumla Kerr (1995) anakiri kuwa iwapo SKM inafuata mfumo wa sanaa za Kiafrika, ni kuzidhalilisha kwani hata sanaa za maonyesho zilizokuwepo kabla ya ukoloni zilikuwa zenye kuweka mizania katika ubora na umbuji na hazikuwa sanaa za hovyo hovyo.

Vile vile, SKM imekuwa kati ya mbinu zinazonyonya amali ya jamii kwa manufaa yake. Kwa mfano, wakati wa kutumia SKM, sanaa na wasanii wanaotumika huwa haviangaliwi. Hakuna uwekezaji unofanyika katika sanaa zaidi ya SKM kujijali yenyewe kama mbinu ya uraghibishi. Ingawa wanalipwa, wasanii wanaoshiriki katika miradi ya SKM kwa muda mrefu wamekuwa wakiathirika na kunyonywa kama jamii inavyonyonywa sanaa yake. Ikiwa lengo la SKM ni kufikisha ujumbe tu na si umbuji wa sanaa yenyewe, au lengo ni mawasiliano na si mchakato wa kuwapatia wasanii stadi za sanaa yenyewe, matokeo yake ni kuwafanya wasanii kuwa tegemezi. Kila msanii mzuri wa sanaa za maonyesho hivi sasa hunyakuliwa na miradi ya SKM kwa ajili ya kupiga baragumu la maradhi, ujinga na umaskini bila kutafakari kuwa yeye ni kati ya watu wanaoshambuliwa na maadui hao wa maendeleo. Ubunifu wa wasanii umemezwa na mifumo ya miradi na hata uhuru wao umefungwa kwani wasanii hawawezi kufanya jambo lolote nje ya andiko la mradi au mtazamo wa wafadhili. Kama Plastow anavyoeleza, kwa sasa SKM hutumika kama mtaji wa watu wanaoandika miradi kwa ajili ya kuomba fedha kwa wafadhili kwa manufaa yao wenyewe na si ya jamii, wasanii au sanaa.

SKM pia imekuwa ikitumiwa kama njia ya kupima maendeleo. Hii inatokana na ukweli kuwa maendeleo yoyote lazima yapimwe kwa vigezo mbali mbali. Upimaji wa maendeleo kwa 'tarakimu na herufi' ndio changamoto kubwa ya dhana nzima ya umaendeleo. Kwa mfano, ikiwa maendeleo ni maji safi, basi ni lazima kujua watu wangapi wameyapata na hao wasiopata ni asilimia ngapi. Hivyo iwapo SKM haitatumiwa kwa uangalifu na uadilifu huweza kupotosha takwimu. Kwa kuwa lengo ni kujua watu wangapi wameona onyesho, wangapi wameuliza maswali na wangapi ni wanawake na wangapi ni wanaume, ni rahisi kupata takwimu za kuridhisha. Changamoto iliyopo ni kuwa SKM mara nyingi haianzishwi na wanajamii wenyewe, bali kundi la waraghibishi/wawezeshaji na watafiti wanaotaka kuiingilia jamii na kutaka kuwaelekeza jinsi ya kuyatambua matatizo yao ambayo mfadhili angependa kuyashughulikia. Hivyo ni rahisi kutumika vibaya kwa ajili ya kumnufaisha mfadhili, mraghibishi au mtafiti.

Mwanzoni nilizungumzia suala la ufuatiliaji na niligusia kuwa wakati mwingine haufanyiki. Ukweli ni kuwa iwapo mfadhili au mtafiti atakuwa amepata taarifa alizokuwa anatafuta hatakuwa na haja ya kurudi kufanya ufuatiliaji. Vile vile iwapo mradi utatenga fungu kwa ajili ya kuwawezesha waraghibishi au watafiti kurudi katika jamii ili kufanya ufuatiliaji na mfadhili akaridhia, basi hilo litafanyika. Lakini kama hakutakuwa na uwezeshwaji wa kufanya ufutiliaji au mradi utakuwa umefika ukingoni, siyo rahisi kwa mtu yeyote kujitolea kurudi kwenye jamii kufanya ufuatiliaji. SKM ni biashara, na kama biashara, ni vizuri kuangalia faida, na kama faida imeshapatikana basi kuna njia mbili; kuboresha biashara kwa kuandika miradi mingi zaidi, au kutumia mtaji kuanzisha biashara mpya. Tabia hii ndiyo hasa inayowaongoza wafadhili, waraghibishi na watafiti kwenda kwenye jamii. Sababu nyingine ni kwa kuwa SKM ya miaka ya sasa imepachikwa tu katika jamii, hata wanajamii hawaoni sababu ya kuendeleza kitu

kisichokuwa chao. Pia mara nyingi katika hatua ya kuchambua matatizo wanajamii wamekuwa wakijitoa na kuwanyooshea viongozi wao vidole kama vikwazo vya maendeleo. Dhana hii ni hatari kwani SKM imeshindwa kusaidia jamii jinsi ya kuwa na viongozi bora na matokeo yake ni kwa viongozi kuichukia jamii ambamo SKM imefanyika (Materego, 2002).

Labda tujiulize, matokeo ya tafiti hizi hupelekwa kwa nani? Kimsingi na kiutendaji, matokeo haya hurudishwa kwa yule aliyetoa pesa za kuwezesha utafiti kufanyika. Na kwa kuwa SKM sasa hivi hufadhiliwa zaidi na wafadhili toka nje kupitia mashirika yasiyo ya kiserikali bila shaka matokeo ya tafiti hizi ndiyo yanayoipa nguvu mifumo ya ubeberu, ubepari na uliberali namna ya kuweza kuendelea kupenyeza 'mirija' yake. Ikumbukwe, mifumo hii imejikita katika kusheheneza matabaka kama njia mojawapo ya kuendelea kuitawala dunia, kwani hata mifumo ya mashirika mengi yasiyo ya kiserikali inalenga katika kuendeleza ubeberu. Igoe & Kelsall (2005) wanasema kuwa dhana ya mashirika yasiyo ya kiserikali ni ya kuendekeza mradi wa uliberali, kitu kinachowaonyesha kama wamisionari wa ukoloni mambo leo – wakala wa ubeberu wa kitamaduni.

Ni wazi kuwa utaratibu wa SKM kumilikiwa na wafadhili unasababisha dhana ya uvamizi wa kiutamaduni kama Freire (1972) alivyotahadharisha. Watafiti na waraghibishi wengi wanalazimika kutumia njia mbalimbali kwa ajili ya kuweka kumbukumbu. Njia hizi ni kamera za picha za mnato na video pamoja na vinasa sauti. Utaratibu huu unapoangaliwa kwa undani haulengi kumpatia mwanajamii husika kumbukumbu hizo, bali mwenye pesa (mfadhili) ili kuthibitisha matumizi ya hela zake. Huu ni utaratibu wa kuwatumia wanajamii kama mashahidi wa matumizi ya pesa, ambazo kwa asilimia kubwa hurudi mifukoni mwa wafadhili na watafiti. Huu ni udhalilishaji unaolenga kuwathibitishia mabepari kuwa kazi imefanyika au inaweza kufanyika kwa uzuri zaidi iwapo watatoa pesa katika msimu wa fedha unaofuata.

Gibbs (1999) ameonyesha wazi kuwa kadri muda unavyokwenda, lengo na manufaa ya SKM yanahama kutoka kwa walengwa ambao ni wananchi kwenda kwa watu binafsi. Hii inatokana na ukweli kuwa matatizo binafsi, mfumo wa uchumi na hasa sera za Benki ya Dunia zimesababisha wanaharakati na wasanii wengi wa Kiafrika kutafuta fedha kutoka kwa wafadhili. Na ni dhahiri kuwa mataifa mengi ya Kiafrika yako katika lindi la madeni na hata dola zimeshindwa kusaidia sanaa na miradi ya maendeleo ya wananchi wao. Ulimwengu (2007) anaangalia dola inayotegemea ufadhili kama dola ya vikaragosi na mateka. Kwani ni dhahiri kuwa utawala wa dunia umejikita kwa wenye nguvu ya kiuchumi. Si rahisi kwa dola inayotegemea ufadhili kuweza kujiamulia mambo yake yenyewe.

Ni dhahiri kuwa tafiti zaidi kuhusu SKM ya kiliberali mamboleo ni muhimu. Ila ni lazima tafiti hizi zilenge kupambana na mifumo ya kisiasa na kiuchumi ya dunia ambayo mara nyingi imekuwa mzigo kwa nchi zinazoendelea kama Tanzania. Siyo sahihi kuamini kuwa SKM ya miaka ya 1980 inaweza kufanyika katika mazingira na utaratibu ule ule wakati ilipobuniwa. Pia ni vizuri kuangalia dhana ya uvamizi wa kitamaduni inavyosanifishwa na SKM badala ya dhana halisi ya umiliki wa SKM. Na ni jambo la muhimu kuhoji sanaa hii inayoitwa Sanaa kwa Maendeleo ili kujua sanaa hii ni kwa maendeleo ya nani – mwanajamii, mtafiti au mfadhili? Kwa kuangalia kijuujuu lengo la SKM ni kumletea mwanajamii maendeleo, ila kwa undani ni kumnyang'anya nguvu inayomwezesha kupata maendeleo yake mwenyewe. Kwa mtazamo wangu, ingawa mfumo wa 'utandawazi' (ubeberu) unalazimisha kuwa 'usipoweza kupambana nao, basi jiunge nao'. Sanaa hata kama imeshindwa kupambana na uliberali mamboleo bado ina nafasi ya kutojiunga nao. Ninaamini sanaa iliyojikita katika kutumia fasihi na kuboresha umbuji inaweza kupambana na mifumo inayotaka kuimeza na kuifanya sehemu ya maslahi ya mifumo hiyo. Na mwisho, kuhusu uhusiano wa SKM na ufadhili, hoja ya msingi inabaki pale pale, "wanja wa manga si dawa ya chongo."

Marejeo

Bakari, J. A., & Materego, G. R. (2008). Sanaa kwa Maendeleo: Stadi, Mbinu na Mazoezi. Moshi: Viva Productions.

Banham, M., Gibbs, J., & Osofisan, F. (Wah.). (1999). African Theatre in Development. Oxford: James Currey Ltd.

Carlson, M. (2001). The Haunted Stage: An Overview. In The Haunted Stage (kur. 1-15). Ann Arbor.

Chachage, C. S., (2003). Nyerere: Nationalism and Post-Colonial Developentalism. Ilichopolewa Januari 20, 2009, kutoka www.codesria.org: http://www.codesria.org/Links/conferences/papers/Chachage_Seithy_L_Chachage.pd

Diagne, S. B., & Ossebi, H. (1996). The Cultural Question in Africa: Issues, Politics and Research Prospects. Dakar: CODESRIA.

Etherton, M. (2004). South Asia's Child Rights Teatre for Development: The Empowerment of Children who are Marginalized, Disadvantaged and Excluded. katika R. Boon, & J. Plastoe (Wah.), Theatre and Empowerment: Community Drama on Stage (kur. 188-218). Cambridge: Cambridge University Press.

Eyoh, H. N. (1984). Hammocks to Bridges: An Experience in Theatre for Development . Yaounde: Yaounde University Research Publication.

Freire, P. (1972). Pedagogy of the Oppressed. Harmondsworth:

Penguin.

Gibbs, J. (1999). Noticeboard. In M. Banham, J. Gibbs, & F. Osofisan (Wah.), African Theatre in Development (kur. 125-126). Oxford: James Currey Ltd.

Igoe, J., & Kelsall, T. (Eds.). (2005). Between a Rock and Hard Place: African NGOs, Donors and the State. Durham: Carolina Academic Press.

Kerr, D. (1995). African Popular Theatre: From Pre-Colonial Times to the Present Day. London: James Currey Ltd.

Lihamba, A. (1985). Politics and Theatre After the Arusha Declaration, 1967-1984. PhD Thesis: University of Leeds.

Materego, G. R. (2002). Popular Theatre in Question: The Issue of Sustainability. MA Dissertation: University of Dar es Salaam.

Mlama, P. (1991). Culture and Development: The Popular Theatre Approach to Africa. Uppsala: Scandnavian Institute of African Studies.

Ndagala, D. K. (2007). Utamaduni na Dhima Yake katika Maendeleo. Dar es Salaam: Tanzania Culture Trust Fund.

Nyerere, J. (1968). Freedom and Socialism. Dar es Salaam: Oxford University Press.

Plastow, J. (2009). Theatre for Development: A Business Opportunity, a Tool of Oppression, or a Road to Empowerment? African Theatre Association-New Directions in African Theatre and Performance. Northampton: AfTA.

Sen, A. (2008). Culture and Development.


Shivji, I. (2007). The Story of Independence: From Nationalism to Neo-liberalism. Sunday Palaver

Ulimwengu, J. (2007). Ili Tuendelee, Hatuhijaji Vitu Vingi. Raia Mwema , October 31.

Kumbukizi: Wasifu Wa Prof. Haroub Miraji Othman [1942 - 2009]

Chris Maina Peter

Profesa wa Sheria, Shule ya Sheria, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Kaimu Mwenyekiti, Bodi ya Wadhamini, Kituo cha Huduma za Sheria, Zanzibar.



Ajuaye hajisifu; hata kama ni sharifu; ajulikana kwa harufu; kuwa yeye ni maarufu!1

Huzuni na Mshituko

Jumapili ya tarehe 28 Juni, 2009 itakumbukwa kama siku isiyo ya kawaida kwa wanachuo wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Zanzibar, Tanzania, Bara la Afrika na jamii ya kimataifa. Ni siku ambayo mwanazuoni maarufu Prof. Haroub Miraji Othman alifariki dunia. Taarifa ya tukio hili lisilo la kawaida ilipokelewa kwa mshituko na mshangao mkubwa. Wengi hawakuamini walilolisikia lakini ukweli ulikuwa huo – kwamba Prof. Haroub Othman ametutoka.

Kilichowachanganya wengi ni ukweli kwamba Prof. Haroub – kama wengi walivyozoea kumwita, hakuwa mgonjwa na jana yake alikuwa ameshiriki kikamilifu katika uzinduzi wa kitabu kuhusu maisha ya Ali Sultan Issa na Seif Sharif Hamad huko Zanzibar. Katika uzinduzi huo alionekana mchangamfu na mwenye mzaha na alikielezea vizuri kitabu hicho kiitwacho Race, Revolution and the Struggle for Human Rights in Zanzibar: Memoirs of Ali Sultan Issa and Seif Sharif Hamad kilichohaririwa na Prof. G. Thomas Burgess. Baada ya hafla hiyo aliondoka na mkewe Profesa Saida Yahya-Othman kuelekea hoteli ya Abuso walikokuwa wamefikia, hoteli iliyoko sehemu ya Shangani, Zanzibar. Kesho yake asubuhi hakuweza kuamka – alikuwa amelala milele.

Historia Fupi ya Prof. Haroub Othman

Prof. Haroub alizaliwa tarehe 30 Novemba, 1942 sehemu ya Msufini, karibu na yalipojengwa sasa maghorofa ya Michenzani mjini Zanzibar. Alisoma katika shule ya French Comorian ya Zanzibar kabla ya kuingia Shule ya Serikali ya Gulioni na baadaye Chuo cha Seyyid Khalifa zote za huko Zanzibar.

Kwa elimu yake ya juu alikwenda Uchina na baadaye Urusi ambako alipata Shahada ya Uzamili ya Sheria (Master of Laws – LL.M) mwaka 1967. Mwaka 1980 alitunukiwa Shahada ya Falsafa ya Sheria (PhD) ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam akiweka rekodi ya kuwa mwanafunzi wa kwanza kutunukiwa shahada hii na Chuo Kikuu cha Dar

[1] Huu ni ubeti katika shairi zuri lililokuwa limetumwa na Mwana UDASA katika anwani ya pamoja likielezea umuhimu wa mtu kuwa wa kiasi katika maisha yake.